

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Telegram "AFYA", DODOMA
Nambari ya Simu: +255 026 – 2323267
E- Mail Na. ps@afya.go.tz



Mji wa Serikali Mtumba,
Barabara ya Afya,
S.L. P 743,
40478 DODOMA.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

TAARIFA YA MWENENDO WA UGONJWA WA CORONA (COVID-19) NCHINI

Dar es Salaam, Ijumaa Aprili 17, 2020

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inatoa taarifa kuwa kati ya sampuli zilizopimwa katika Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii jana tarehe 16 Aprili, 2020 na leo Aprili 17, 2020 zinaonyesha kuwepo kwa **wagonjwa wapya 53** wenye maambukizi ya virusi vya Corona (COVID-19) nchini.

Wagonjwa hawa wote ni watanzania ambao wameripotiwa katika mikoa ya **Dar es Salaam (38)**, **Kilimanjaro (1)**, **Mwanza (1)**, **Pwani (1)**, **Lindi (1)** na **Kagera (1) wakati wagonjwa (10)** wameripotiwa kuwepo **Zanzibar**. Aidha, tunasikitika kutangaza kifo cha mtu mmoja (1) kilichotokana na ugonjwa wa Corona nchini.

Hivyo hadi sasa kuna jumla ya watu **147** waliopata maambukizi ya virusi vya Corona (**COVID – 19**) nchini, kati yao waliopona ni **11** na vifo **5** vimethibitishwa tangu kuanza kuripotiwa kwa ugonjwa huu nchini tarehe 16 Machi 2020. Wagonjwa wote **waliobaki (131)** **hali zao** ni nzuri isipokuwa wanne **(4)** ambao wanapatiwa matibabu ya wagonjwa mahututi kutokana na kuwa wana wanasumbuliwa na matatizo mengine ya kiafya.

Aidha, tumebaini kuwa wapo watu wenye dalili za ugonjwa wa Corona wanaokwenda kupata huduma za matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili. Hospitali hii ndiyo hospitali kuu ya rufaa ya kitaifa kwa wagonjwa wa magonjwa mengine nchini ambayo pia inatoa matibabu ya kibingwa na matibabu bobezi ikiwemo upasuaji mkubwa, upandikizaji wa figo na vifaa vya kusaidia kusikia kwa watoto, upasuaji wa mifupa na mishipa ya fahamu na matibabu ya magonjwa ya moyo. Hivyo, Serikali imeelekeza Hospitali ya Taifa Muhimbili kuacha kupokea wagonjwa wenye dalili za virusi vya Corona (Covid-19). Wananchi wenye dalili za ugonjwa huu **wanatakiwa kuacha kwenda Hospitali ya Taifa Muhimbili** kwa ajili ya huduma za matibabu ya corona.

Badala yake Serikali imeamua kutumia Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Amana (Dar es Salaam) kama kituo maalum cha matibabu ya ugonjwa wa CODIV-19. Wananchi wa mkoa wa Dar es Salaam wanaohitaji kupata huduma za matibabu ya magonjwa mengine katika Hospitali ya Amana wanatakiwa kutumia hospitali nyingine zilizopo mkoani hapa.

Kipekee kwa niaba ya Serikali natoa shukrani za dhati kwa watumishi wa afya hasa walio mstari wa mbele katika kutoa huduma katika kipindi hiki cha mlipuko wa COVID-19 nchini. Aidha, tunatoa shukrani za dhati kwa makampuni binafsi na wadau wa maendeleo kwa michango mbali mbali wanayoitoa kwa Serikali katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa huu.

Napenda kuwakumbusha wananchi kuendelea kuzingatia na kufuatilia maelekezo ya wataalam wa afya katika kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huu ikiwa ni pamoja na kunawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka, kuepuka misongamano na kukaa umbali wa zaidi ya mita moja baina ya mtu na mtu. Wananchi wenyewe dalili za ugonjwa wa Corona (COVID-19) wanashauriwa kuwahi hospitali kupata ushauri na huduma ya afya na kujitenga ili kuepuka kusambaza maambukizi kwa wengine.



Ummy A. Mwalimu (Mb)
**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO**